

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Anwani ya Simu: "ELIMU" DAR
ES SALAAM

Simu: +255 22 2110146-10

Baruapepe: info@moe.go.tz

Nukushi: +255 22 2135486

Tovuti: www.moe.go.tz

Unapojibu Tafadhali Taja

Kumb. Na. TTDB. 193/216/01/113



7 Mtaa wa Magogoni,

S.L.P. 9121,

11479 DAR ES SALAAM.

Tarehe: 10/11/2016

Makatibu Tawala wa Mikoa,
Wathibiti Ubora Wakuu wa Shule wa Kanda,
Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji,
Wakuu wa Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali,
TANZANIA BARA.

**WARAKA WA ELIMU NA. 5 WA MWAKA 2016
MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA
MAFUNZO YA UALIMU**

Kuanzia mwaka wa masomo 2014/15, Wizara ilihushia programu za mafunzo ya Ualimu ili kukidhi mahitaji ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Kwa sasa, Wizara inaendelea na maandalizi ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya utekelezaji wa Sera hii ikiwemo uendeshaji na usimamizi wa mafunzo ya Ualimu nchini.

Kwa kuzingatia maandalizi yanayoendelea, mwongozo wa utekelezaji wa programu za mafunzo ya ualimu kuanzia mwaka 2016/2017 utakuwa kama ifuatavyo:

- i. Programu za mafunzo ya Ualimu zitakuwa Astashahada (Cheti) na Stashahada. Mafunzo haya yataendeshwa kwa kutumia Mtaala wa Kitaifa ulioandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania wa mwaka 2009 kwa Astashahada (Cheti) na Stashahada;
- ii. Wizara itakuwa inatoa maelekezo ya sifa za kujiunga na mafunzo ya Ualimu;
- iii. Mafunzo Tarajali ya Stashahada ya Juu ya Elimu ya Sekondari yaliyokuwa yakitolewa kuanzia mwaka wa masomo 2014/15 yamehitimishwa. Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) litatoa tuzo ya Stashahada ya

- Kawaida ya Ualimu wa Sekondari kwa wahitimu wa programu hii baada ya kukamilisha mwaka wa pili wa masomo;
- iv. Wanachuo wanaoendelea na Mafunzo Tarajali ya Ualimu wa Stashahada ya Kawaida kwa kutumia Mtaala wa Tuzo za Taifa za Elimu ya Ufundi (NTA) wataendelea na mafunzo yao na kuhitimisha kama ilivyopangwa;
 - v. Programu ya mafunzo kazini ya Stashahada ya Elimu ya Msingi iliyokuwa inatumia Mtaala wa Tuzo za Taifa za Elimu ya Ufundi (NTA) imesitishwa ili kufanyiwa maboresho;
 - vi. Baraza la Mitihani la Tanzania litatahini na kutoa tuzo ya mafunzo ya Ualimu ya Astashahada (Cheti) na Stashahada kuanzia mwaka wa masomo 2016/17; na
 - vii. Vyuo vya Ualimu vihusike kutoa mafunzo ya Ualimu (Astashahada na Stashahada) pekee bila kuchanganya na kozi zingine.

Waraka huu unaanza kutumika katika mwaka wa masomo 2016/17 katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali.

Nawatakia utekelezaji mwema.



Nicolas J. Buretta

KAIMU KAMISHNA WA ELIMU

Nakala: Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
DAR ES SALAAM

Katibu Mtendaji
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624
DAR ES SALAAM

Katibu Mtendaji
Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.
S.L.P. 7109
DAR ES SALAAM

Katibu Mtendaji
Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania
S.L.P 6562
DAR-ES-SALAAM